

»Jinsi ya kukuza celery kutoka kwa mbegu»

Celery ni mboga ya majani ambayo hustahimili hali ya baridi, joto na kivuli. Celery ni maarufu sana na hukuzwa kwa ajili ya ladha na mabua yake laini na pia. Mmea huo huathiriwa na magonjwa machache na hauhitaji shughuli nydingi. Hata hivyo, joto linapoongezeka sana hushusha ubora wake.

Kukuza celery kunahitaji hatua rahisi, na kawaida celery zilizopandwa nyumbani huwa zina ladha zaidi na afya. Mbegu za celery huota kati ya wiki 2 hadi mwezi, na hukua polepole. Kwa hivyo anza kupanda mbegu miezi miwili na nusu kabla ya msimu wa upandaji. Epuka jua ya moja kwa moja wakati wa kupanda, kufanya huku kunasababisha mashina mrefu na laini. Kupandikiza kunapaswa kufanywa katika wiki ya nne.

Hatua

Loweka mbegu kwa masaa 12, funga mbegu kwa karatasi. Weka karatasi ndani ya mfuko wa plastiki na uweke kwenye jokofu kwa masaa 24 ili kuhimiza uotaji.

Panda mbegu kwenye viriba, na endelea kumwagilia maji kwani mbegu huchukua muda mrefu kuota.

Tenganisha miche na uweke kila mmoja kwenye kiriba tofauti.

Funika mizizi na mchanganyiko wa udongo, kisha mwagilia maji mara kwa mara ili miche ikue vizuri.

Panda celery kwa umbali wa nusu futi, kwa kuwa upandaji wa karibu husababisha mabua mafupi na mazito.

Baada ya kupandikiza, mwagilia maji vizuri kwa ukuaji sahihi.

Weka mboji na uongeze mbolea ya madini iwapo inahitajika.

Kata mashina makubwa kwa chakula, na acha mmea utoe mabua
mapya au uvune mmea mzima.